URANI YA MTO MKUJU

# Urithi unaoweka Tanzania katika ramani mpya kidunia

Na Albano Midelo

WANANCHI wa Kata ya Likuyu wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma wanapakana na Mradi wa Madini ya Urani katika Mto Mkuju, sauti za ndege zinazochanganyika na kelele za magari mazito yanayopita kuelekea eneo la mradi.

Kwa macho ya kawaida, huenda eneo hilo likaonekana kama sehemu nyingine ya vijijini Tanzania.

Lakini chini ya ardhi yake kuna hazina inayoweza kubadilisha historia ya uchumi wa Tanzania, nafasi yake katika sekta ya madini duniani, na mchango wake katika mapambano ya kimataifa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Madini ya urani ambayo kwa miongo mingi yamekuwa yakihusishwa na teknolojia za kisasa za nishati duniani, sasa yanaibuka kama fursa mpya ya maendeleo kwa Tanzania kupitia Mradi wa Urani wa Mto Mkuju unaotarajiwa kuifanya nchi kuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa urani duniani.

Katika kipindi ambacho dunia inapambana kutafuta vyanzo vya nishati safi vinavyoweza kupunguza utegemezi wa mafuta na makaa ya mawe, Tanzania inajiandaa kuingia katika ramani ya mataifa yanayochangia suluhisho la changamoto hiyo kupitia rasilimali zake za madini.

Hazina inayoweza ubadilisha uchumi wa taifa

Kwa mujibu wa Meneja wa Mradi wa Mto Mkuju, Beria Vorster utakapokamilika na kuanza uzalishaji wa kibiashara, mradi huo unatarajiwa kuchangia takribani asilimia nne ya uzalishaji wote wa urani duniani.

Takwimu hizo zinaonesha ukubwa wa mradi huo kwa kiwango cha kimataifa.

Kwa mujibu wa Ripoti ya World Nuclear Association ya mwaka 2024, Kazakhstan ndiyo ilikuwa kinara wa uzalishaji wa urani duniani kwa kuchangia asilimia 39 ya uzalishaji wote wa dunia, ikifuatiwa na Canada kwa asilimia 24, Namibia asilimia 12, Uzbekistan asilimia 7 huku Urusi ikichangia kati ya asilimia nne hadi tano.

Iwapo makadirio ya Mradi wa Mto Mkuju yatatekelezwa kama ilivyopangwa, Tanzania inaweza kuingia katika orodha ya nchi 10 bora duniani zinazozalisha urani.

Jambo hilo litakuwa mafanikio makubwa katika historia ya sekta ya madini nchini.

Hii ni hatua kubwa ukizingatia kwamba kwa sasa nchi nyingi za Afrika Mashariki bado hazina migodi mikubwa ya urani inayozalisha kwa kiwango cha kibiashara.




Rais Samia Suluhu Hassan alipozindua kiwanda cha majaribio cha kuchenjua madini ya urani katika eneo la Mto Mkuju, Namtumbo mkoani Ruvuma Julai 2025.

**Dunia inahitaji urani kuliko zamani**

Katika miaka ya hivi karibuni, mjadala wa nishati duniani umebadilika kwa kasi.

Ripoti ya Shirika la Kimataifa la Nishati (IEA) ya Mwaka 2024 inaonesha mahitaji ya umeme duniani yanatarajiwa kuongezeka kwa zaidi ya asilimia 60 ifikapo mwaka 2050 kutokana na ongezeko la watu, maendeleo ya viwanda na matumizi ya teknolojia za kisasa.

Wakati huo huo, Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mabadiliko ya Tabianchi (UN Climate Change) linaendelea kusisitiza umuhimu wa kupunguza uzalishaji wa gesi chafuzi ili kufikia malengo ya Mkataba wa Paris.

Kutokana na hali hiyo, nchi nyingi zimeanza kuwekeza zaidi katika nishati ya nyuklia inayozalisha kiwango kidogo cha hewa ukaa ikilinganishwa na makaa ya mawe au mafuta.

Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA), zaidi ya asilimia 10 ya umeme wa dunia huzalishwa kupitia nishati ya nyuklia, huku nchi kama Ufaransa zikipata zaidi ya asilimia 60 ya umeme wake kutoka katika vyanzo hivyo.

Hii ndiyo sababu urani imeendelea kuwa madini muhimu katika ajenda ya nishati safi duniani.

**Ukweli kuhusu hofu ya silaha za nyuklia**

Moja ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara na wananchi ni kama urani inayochimbwa Tanzania inaweza kutumika kutengeneza silaha za nyuklia.

**Jibu ni hapana.**

Vorster anafafanua kuwa urani ya Mto Mkuju itatumika katika uzalishaji wa nishati safi kupitia mitambo ya kuzalisha umeme wa nyuklia na si kwa ajili ya silaha.

Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Kuzuia Uenezaji wa Silaha za Nyuklia (NPT) unaoweka masharti makali ya usimamizi wa matumizi ya madini hayo.

Aidha, Shirika la Kimataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA) lina mifumo madhubuti ya ukaguzi na ufuatiliaji wa matumizi ya urani duniani kuhakikisha inatumika kwa madhumuni ya amani na maendeleo.

**Mabilioni ya dola na maelfu ya ajira**

Mbali na umuhimu wake wa kimkakati duniani, mradi huo unatarajiwa kuwa injini mpya ya uchumi wa Tanzania.

Akizungumza katika uzinduzi wa kiwanda wa majaribio cha kuchenjua urani, Mto Mkuju Namtumbo mkoani Ruvuma Julai 30, 2025, Rais Samia Suluhu Hassan anasema mradi huo unatarajiwa kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.2.

Kwa mujibu wa tathmini ya serikali, mradi huo utadumu kwa miaka 20.

Katika kipindi hicho, ajira takribani 3,500 zinatarajiwa kupatikana wakati wa ujenzi wa miundombinu ya mradi, ajira za kudumu 750 wakati wa uzalishaji pamoja na ajira zaidi ya 4,500 zitakazotokana na shughuli nyingine za kiuchumi zinazohusiana na mradi.

Serikali pia inatarajia mapato makubwa kupitia mrabaha wa Dola za Marekani milioni 373, kodi ya kampuni inayokadiriwa kufikia Dola za Marekani bilioni 1.01, pamoja na mapato mengine yatokanayo na kodi na gawio la serikali.

Kwa wataalamu wa uchumi, takwimu hizo zinaashiria mchango mkubwa katika ukuaji wa pato la taifa, mapato ya serikali na maendeleo ya maeneo yanayozunguka mradi.

**Sauti kutoka Namtumbo**

Kwa miaka mingi, baadhi ya wananchi wa Namtumbo walikuwa wakikabiliwa na changamoto za ukosefu wa ajira na fursa chache za kiuchumi.

Mkazi wa kijiji cha Likuyu Mohamed Ally Hassan anasema hali hiyo imeanza kubadilika.

"Zamani vijana walikuwa wanamaliza shule na kubaki nyumbani bila kazi. Tangu shughuli za mradi zianze, tumeshuhudia watu wakipata mafunzo na wengine kupata ajira," anasema na kuongeza: "Tunatarajia ajira zitaongezeka zaidi uzalishaji utakapoanza rasmi."

**Nafasi ya Tanzania**

Katika Afrika Mashariki, Tanzania ina nafasi ya kipekee kutokana na ukubwa wa rasilimali za urani zilizogunduliwa Mto Mkuju.

Nchi nyingi za ukanda huo zimejikita zaidi katika madini ya dhahabu, shaba, kobalti na mafuta, huku urani ikiwa bado haijachukua nafasi kubwa katika uzalishaji wa kibiashara.

Kwa kiwango cha Afrika, Namibia na Niger zimekuwa miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa urani kwa miaka mingi.

Hata hivyo, wataalamu wanaamini kuwa, kuanza kwa uzalishaji wa Mto Mkuju kutaimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu kipya cha uwekezaji wa madini ya kimkakati barani Afrika.

**Sheria, sera na miongozo**

Mafanikio ya mradi huu yanategemea pia usimamizi madhubuti wa sheria na sera.

Miongoni mwa nyaraka muhimu zinazosimamia shughuli hizi ni Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, Sera ya Taifa ya Madini ya Mwaka 2009 pamoja na miongozo ya Shirika la Kimataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA).

Rais Samia anasisitiza umuhimu wa kampuni inayotekeleza mradi huo kuhakikisha kipaumbele kinatolewa kwa Watanzania, hasa wananchi wa maeneo yanayouzunguka mradi.

**Tanzania tayari kwa enzi mpya**

Swali hili limeendelea kujitokeza kadri maandalizi ya uzalishaji yanavyoendelea.

Kutokana na ukubwa wa uwekezaji, nafasi ya Tanzania katika soko la dunia, ongezeko la ajira na mapato ya serikali, wachambuzi wanaamini kuwa Mradi wa Mto Mkuju unaweza kuwa miongoni mwa miradi ya kimkakati yenye athari kubwa zaidi katika uchumi wa Tanzania katika karne hii.

Hata hivyo, mafanikio yake yatategemea usimamizi bora wa mazingira, ushirikishwaji wa wananchi, uwazi katika matumizi ya mapato yatakayopatikana na uwekezaji katika elimu na ujuzi wa Watanzania.

**Ruvuma na historia mpya ya Tanzania**

Wakati dunia ikiendelea kutafuta suluhisho la changamoto za nishati na mabadiliko ya tabianchi, eneo la Mto Mkuju lililokuwa kimya kwa miaka mingi sasa linaanza kusikika katika ramani ya kimataifa.

Chini ya ardhi ya Namtumbo mkoani Ruvuma kuna madini yanayoweza kufanya Tanzania kuwa mchezaji muhimu katika sekta ya nishati safi duniani.



Sehemu ya mradi wa kiwanda cha kuchenjua madini ya urani katika eneo la Mto Mkuju, Namtumbo mkoani Ruvuma.